**HOTUBA YA IJUMAA**

**الزكاة والصدقات ودورهما في التنمية المجتمعية**

**Zaka na Sadaka na nafasi zake katika maendeleo ya jamii**

**Imefasiriwa**

**Na**

**Profesa.Ayman Alasar**

Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mwenye kusema ndani ya Kitabu chake Kitukufu: **وَأَقِيمُوا الصَّلاةَ وَآتُوا الزَّكَاةَ وَارْكَعُوا مَعَ الرَّاكِعِينَ** {**Na shikeni Sala na toeni Zaka, na inameni pamoja na wanao inama**}. Ninashuhudia kuwa hakuna mola wa anayepaswa kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu peke yake hana mshirika, na ninashuhudia kuwa Mtume wetu Muhammad ni Mtume wake na mja wake. Ewe Mwenyezi Mungu peleka rehma na amani pamoja na baraka kwake Mtume na kwa watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake na wale wanaowafuata kwa wema mpaka siku ya Kiyama.

Baada ya utangulizi:

Sharia ya Kiislamu imewawekea watu mfumo thabiti wa kijamii, msingi wake ni kufanyiana huruma na kushikamana, ambapo Mtume SAW anasema:

**مَثَلُ الْمُؤْمِنِينَ فِي تَوَادِّهِمْ، وَتَرَاحُمِهِمْ، وَتَعَاطُفِهِمْ مَثَلُ الْجَسَدِ إِذَا اشْتَكَى مِنْهُ عُضْوٌ تَدَاعَى لَهُ سَائِرُ الْجَسَدِ بِالسَّهَرِ وَالْحُمَّى.**

"*Mfano wa Waumini katika kupendana kwao na kufanyia kwao huruma ni kama mfano wa mwili mmoja pindi kiungo kimoja kinapohisi maumivu basi viungo vilivyobaki havipati usingizi kwa kuhisi homa*", na Mtume SAW anasema:

إِنَّ الْأَشْعَرِيِّينَ إِذَا أَرْمَلُوا فِي الْغَزْوِ أَوْ قَلَّ طَعَامُ عِيَالِهِمْ بِالْمَدِينَةِ؛ جَمَعُوا مَا كَانَ عِنْدَهُمْ فِي ثَوْبٍ وَاحِدٍ ثُمَّ اقْتَسَمُوهُ بَيْنَهُمْ فِي إِنَاءٍ وَاحِدٍ بِالسَّوِيَّةِ، فَهُمْ مِنِّي وَأَنَا مِنْهُمْ.

"*Watu wa kabila la Al-Ash'ar pindi wanapoishiwa na mahitaji yao u kupungukiwa chakula cha watoto wao wakiwa vitani hukusanya kichache walichobakiwa nacho kwenye nguo moja kisha wanagawana ndani ya chombo kimoja kati yao kwa usawa basi wao ni sehemu yangu na mimi ni sehemu kwao*".

Hivyo Uislamu umeweka Sharia ya zaka na kuifanya ni katika nguzo zake, na kuhimiza utoaji wa sadaka na kuifanya ni katika mlango mkubwa wa mambo ya kheir kutokana na kuchangia katika kukidhi mahitaji ya wenye kuhitaji, na kuwandolea matatizo yao ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu Anasema:

خُذْ مِنْ أَمْوَالِهِمْ صَدَقَةً تُطَهِّرُهُمْ وَتُزَكِّيهِمْ بِهَا .

{**Chukua sadaka katika mali zao, uwasafishe na uwatakase kwazo**}. Na Mola Mtukufu Anaendela kusema: وَمَا أَنْفَقْتُمْ مِنْ شَيْءٍ فَهُوَ يُخْلِفُهُ وَهُوَ خَيْرُ الرَّازِقِينَ {**Na chochote mtakacho kitoa Yeye atakilipa. Naye ni Mbora wa wanao ruzuku**}. Na Mtume wetu Muhammad SAW anasema:

بُنِيَ الإِسْلَامُ عَلَى خَمْسٍ: شَهَادَةِ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَأَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللَّهِ، وَإِقَامِ الصَّلَاةِ، وَإِيتَاءِ الزَّكَاةِ، وَالحَجِّ، وَصَوْمِ رَمَضَانَ.

"*Uislamu umejengwa kwenye nguzo tano: Kushuhudia kuwa hakuna mola wa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu na Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, kudumisha swala kutoa zaka kutekeleza ibada ya hija na kufunga funga ya mwezi wa Ramadhani*".

Mwenye kuzingatia ndani ya Quran Tukufu atakuta kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu sehemu nyingi amekutanisha zaka na ibada kubwa na tukufu yao na yenye sehemu kubwa nayo ni ibada ya swala ikiwa ni kutukuza uzito wa zaka, na hilo likiwa ni kuipendezesha kwenye kuitekeleza kwake ambapo Mola Mtukufu anasema: وَأَقِيمُوا الصَّلاَةَ وَآتُواْ الزَّكَاةَ وَمَا تُقَدِّمُواْ لأَنفُسِكُم مِّنْ خَيْرٍ تَجِدُوهُ عِندَ اللّهِ إِنَّ اللّهَ بِمَا تَعْمَلُونَ

بَصِيرٌ {**Na shikeni Sala na toeni Zaka; na kheri mtakazojitangulizia nafsi zenu mtazikuta kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu anayaona mnayo yafanya**}. Na Mwenyezi Mungu anaendelea kusema:

**الَّذِينَ يُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ وَهُم بِالْآخِرَةِ هُمْ يُوقِنُونَ.**

{**Wanao shika Sala, na wanatoa Zaka, nao wana yakini na Akhera**}. Kama vile Sharia imekuja na tahadhari ya kudharau utoaji zaka ambapo Mola Mtukufu anasema:

**وَلَا يَحْسَبَنَّ الَّذِينَ يَبْخَلُونَ بِمَا آتَاهُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ هُوَ خَيْرًا لَهُمْ بَلْ هُوَ شَرٌّ لَهُمْ سَيُطَوَّقُونَ مَا بَخِلُوا بِهِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَلِلَّهِ مِيرَاثُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ.**

{**Wala wasidhani wale ambao wanafanya ubahili katika aliyo wapa Mwenyezi Mungu katika fadhila zake kuwa ni kheri kwao. Bali hiyo ni shari kwao. Watafungwa kongwa za yale waliyo yafanyia ubahili Siku ya Kiyama. Na urithi wa mbingu na ardhi ni wa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu anazo habari za yote myatendayo**}. Na Mola Mtukufu anaendela tena kusema:

**وَالَّذِينَ يَكْنِزُونَ الذَّهَبَ وَالْفِضَّةَ وَلَا يُنْفِقُونَهَا فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَبَشِّرْهُمْ بِعَذَابٍ أَلِيمٍ * يَوْمَ يُحْمَى عَلَيْهَا فِي نَارِ جَهَنَّمَ فَتُكْوَى بِهَا جِبَاهُهُمْ وَجُنُوبُهُمْ وَظُهُورُهُمْ هَذَا مَا كَنَزْتُمْ لِأَنْفُسِكُمْ فَذُوقُوا مَا كُنْتُمْ تَكْنِزُونَ.**

{**Na wanao kusanya dhahabu na fedha, wala hawazitumii katika Njia ya Mwenyezi Mungu, wabashirie habari ya adhabu iliyo chungu * Siku zitapo tiwa moto katika Moto wa Jahannamu, na kwazo vikachomwa vipaji vya nyuso zao na mbavu zao na migongo yao, wakaambiwa: Haya ndiyo mlio jilimbikizia nafsi zenu, basi onjeni mliyo kuwa mkilimbikiza**}. Na Abdillah Ibn Abbas R.A anasema: Aya tatu zimekutana na mambo matatu, wala Aya moja haikubali bila ya nyengine Aya ya kwanza: **وَأَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُول** {**Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume**} hivyo mwenye kumtii Mwenyezi Mungu bila ya kumtii Mtume basi utiifu wake haukubaliki, na Aya ya pili: **وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَآتُوا الزَّكَاةَ** {**Na shikeni swala na toeni zaka**} hivyo mwenye kuswali na wala asitoe zaka basi swala yake

haitokubaliwa, na Aya ya tatu: أَنِ اشْكُرْ لِي وَلِوَالِدَيْكَ {**Unishukuru Mimi na wazazi wako**} mwenye kumshukuru Mwenyezi Mungu pasi ya kuwashukuru pia wazazi wake basi shukrani zake hazitokubalika.

Hakuna shaka kuwa sadaka inaungana na zaka katika kufikia nafasi yake kijamii, hivyo Sharia imekuja kuhimiza ibada ya sadaka, ambapo Mtume wetu SAW anasema: **إِنَّ فِي الْمَالِ لَحَقًّا سِوَى الزَّكَاةِ** "*Kwa hakika katika mali kuna haki isiyokuwa ya zaka*" kisha akasoma kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu:

**لَيْسَ الْبِرَّ أَنْ تُوَلُّوا وُجُوهَكُمْ قِبَلَ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ وَلَكِنَّ الْبِرَّ مَنْ آمَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَالْمَلَائِكَةِ وَالْكِتَابِ وَالنَّبِيِّينَ وَآتَى الْمَالَ عَلَى حُبِّهِ ذَوِي الْقُرْبَى وَالْيَتَامَى وَالْمَسَاكِينَ وَابْنَ السَّبِيلِ وَالسَّائِلِينَ وَفِي الرِّقَابِ...**

{**Sio wema kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa mashariki na magharibi. Bali wema ni wa anaye muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho na Malaika na Kitabu na Manabii, na anawapa mali, kwa kupenda kwake, jamaa na mayatima na masikini na wasafiri, na waombao, na katika ugombozi**}.

*****

**HOTUBA YA PILI.**

Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, rehma na amani vimshukie Mtume wa mwisho naye ni Mtume wetu Muhammad SAW pamoja na watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake wote.

Ibada ya zaka na sadaka ni zenye faida kubwa, miongoni mwazo:

Kupata baraka na malipo makubwa ambapo Mola Mtukufu anasema: **يَمْحَقُ اللَّهُ الرِّبَا وَيُرْبِي الصَّدَقَاتِ** {**Mwenyezi Mungu huiondolea baraka riba, na huzibariki sadaka**}. Na anasema tena:

**إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَآتَوُا الزَّكَاةَ لَهُمْ أَجْرُهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ.**

{**Hakika wale walio amini na wakatenda mema na wakashika Sala na wakatoa Zaka, wao watapata malipo yao kwa Mola wao Mlezi, wala haitakuwa hofu juu yao, wala hawatahuzunika**}. Na Mtume SAW anasema:

**مَا مِنْ يَوْمٍ يُصْبِحُ الْعِبَادُ فِيهِ إِلَّا مَلَكَانِ يَنْزِلَانِ، فَيَقُولُ أَحَدُهُمَا: اللهُمَّ أَعْطِ مُنْفِقًا خَلَفًا، وَيَقُولُ الْآخَرُ: اللهُمَّ أَعْطِ مُمْسِكًا تَلَفًا .**

"*Hakuna siku waja wanaamika nayo isipokuwa kuna Malaika wawili wanateremka, mmoja wao anaomba kwa kusema: Ewe Mwenyezi Mungu mpa mwenye kutoa badala ya alichokitoa, na Malika mwengine anaomba kwa kusema: Ewe Mwenyezi Mungu mpe mwenye kujizuia kutoa uharibifu wa mali yake au kuangamia mali zake*".

Pia: Zenyewe ni sababu miongoni mwa sababu za afya kwani Mtume SAW anasema: **دَاوُوا مَرْضَاكُمْ بِالصَّدَقَةِ، وَحَصِّنُوا أَمْوَالَكُمْ بِالزَّكَاةِ، وَأَعِدُّوا لِلْبَلَاءِ الدُّعَاءَ** "*Wafanyieni dawa wagonjwa wetu kwa kutoa sadaka, na linden mali zenu kwa kutoa zaka, na ondoeni matatizo kwa kufanya maombi*". Na Mtume SAW anaendelea kusema:

**إِنَّ الصَّدَقَةَ تُطْفِئُ غَضَبَ الرَّبِّ وَتَدْفَعُ مِيتَةَ السُّوءِ.**

"*Hakika sadaka huzima hasira za Mola wangu na kuondoa uovu*".

Ibada ya zaka ina nafasi kubwa katika kufikia uwiano wa kijamii na kufikia maendeleo ya kijamii, na inakunjua kwa sehemu kubwa katika maswala ya sadaka ni sawa sawa sadaka za kuendelea au sadaka za wote au katika sura ya ujenzi wa miradi ya kulisha chakula au miradi ya uzalishaji mavazi na ujenzi wa makazi au kuimarisha nafasi za kazi na miradi mengine ya mambo ya heri ambayo inachangia katika kufikia usimamizi wa kibinadamu wa kifamilia au kwa maendeleo ya kijamii.

Ni wenye kuhitaji sna kufikia maana za wema na mshikamano wa kijamii ili upendo uweze kuenea pamoja na undugu na kufikia maendeleo.

Ewe Mwenyezi Mungu ihifadhi nchi yetu ya Misri pamoja na ulimwengu wa Kiislamu na Kiarabu.